# ACADEMIC BREAKTHROUGH SERIES

SASON 002

## DARASA LA 7 - MWAKA: 2021

## KISWAHILI: LUGHA

**Muda: Saa 1 Dak. 40**

***Chagua jibu mwafaka kujaza nafasi 1 - 15.***

Jamii __1__ huhitaji __2__ ya makuzi ya watoto. Hoja ya wazazi __3__ kujitafutia mali kiholela __4__ iwe ni kuwatambua __5__ wa mali inayotafutwa. Hii ndiyo maana wazazi __6__ leo hujitahidi kuisimamisha misingi __7__ malezi bora ya watoto __8__ kuwasomesha.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. thabiti | B. tabithi | C. dhabiti | D. tabithi |
| 2. | A. mathubuti | B. matubuthi | C. madhubuti | D. thabiti |
| 3. | A. iwe tu | B. isikuwe tu | C. isiwe tu | D. asiye tu |
| 4. | A. bali | B. seuze | C. madhali | D. kefu |
| 5. | A. waridhi | B. warihi | C. waridhi | D. warithi |
| 6. | A. wengi | B. wingi | C. nyingi | D. mengi |
| 7. | A. za | B. ya | C. wa | D. na |
| 8. | A. na | B. kwa | C. pa | D. wa |

Niligutushwa kutoka usingizi wa __9__ na ndoto ya __10__. Majoka __11__ nusura yanimeze! Joto __12__ mwilini lilisababisha __13__ na jasho. Sikuelewa maana ya __14__ hilo. Nilijipinda na kujaribu kupata __15__ lepe la usingizi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9. | A. mang'amung'amu | B. pono | C. mtamu | D. mzito |
| 10. | A. kutishiwa | B. kutishiya | C. kufurahia | D. kutisha |
| 11. | A. mbili | B. wawili | C. mawili | D. miwili\ |
| 12. | A. lingi | B. mingi | C. nyingi | D. jingi |
| 13. | A. kotokea | B. kutoroka | C. kutokwa | D. kutoa |
| 14. | A. ruiya | B. kaputi | C. njozi | D. jinamizi |
| 15. | A. angalau | B. aghalabu | C. hasa | D. hata |

***Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. "Chewa" ni salamu za wakati gani?
A. Wowote B. Usiku C. Asubuhi D. Jioni

17. Nomino inayotokana na kitenzi **aka** ni ______
A. washa B. asha
C. mwasho D. mwashi

18. Bainisha maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi ifuatayo:
Kelbu **yule** ni wangu **huyu** ni wake.
A. Kiashiria kielezi
B. Kiwakilishi kiashiria
C. Kitenzi kiwakilishi
D. Kivumishi kiwakilishi

19. Mwanzele amemwoa Ashina. Daudi akamwoa Saumu. Mwanzele na Daudi wamekuwa marafiki wa hali na mali. Je, wataitanaje ikiwa Ashina na Saumu ni ndugu wa toka nitoke?
A. Sotho B. Wandani C. Mkoi D. Mwanyumba

20. Kanusha:
Mimi hula chakula kingi.
A. Mimi sijala chakula kingi
B. Mimi huwa sili chakula kingi
C. Mimi sikula chakula kingi
D. Mimi sili chakula haba

21. Je, akisami hii $^2/_5$ ni
A. humusi mbili B. nusu tano
C. humusi nusu D. robo tano

22. Jina jingine la "Mungu" ni
A. Suheli B. Dayani
C. Karia D. Shimali

23. Kitenzi "Lewa" katika kauli ya kutendesha ni
A. Levya B. Leweka C. Lezwa D. Lewalewa

24. Sentensi ipi ni sahihi kisarufi?
A. Nyuso haya zinapendeza
B. Nyuso hii inapendeza
C. Nyuso hizi inapendeza
D. Nyuso hizi zinapendeza

25. Andika kwa wingi:
Ukuta huu una ufa mrefu.
A. Kuta hizi zina ufa ndefu
B. Kuta hizi zina nyufa mrefu
C. Kuta hizi zina nyufa ndefu
D. Ukuta mrefu zina nyufa mrefu


26. Kikembe cha nyuki ni jana je; kikembe cha chura ni
A. kiluwiluwi
B. kihongwe
C. kimatu
D. kichura

27. Jibu gani lina nomino ambazo ziko katika ngeli ya YA - YA pekee?
A. Maji manukato
B. Maembe mate
C. Mkate mali
D. Mizani sukari

28. Tambua tamathali ya lugha iliyotumika katika sentensi ifuatayo.
Sidi ni msiri kama usiku.
A. Tashbihi
B. Methali
C. Istiari
D. Nahau

29. Andika tarakimu hii kwa maneno.
**300303**
A. Laki tatu mia tatu na tatu
B. Laki mia tatu mia tatu na tatu
C. Laki tatu elfu tatu na tatu
D. Laki tatu, na tatu, mia tatu

30. Taja majina ya maumbo yafuatayo.



A. Mche mraba, mstari sambamba
B. Mstatili, mstari sulubu
C. Mche mstatili, mstari sambamba
D. Mche, mstari sulubu

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 31 - 40.</u>***

Elimu ni mwanga wa taifa. Insi wengi walioelimika hutumia ujuzi na ustadi wao kuzalisha **<u>rasilimali</u>** nchini. Waja hawa huchangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya kiuchumi nchini. Jinsi nchi ilivyoimarika kiuchumi.

Kijamii, elimu huinua kiwango cha maisha cha watu. Watu walioelimika huweza kupata **<u>ajira</u>** na mapato wayapatayo huwasaidia kujikimu vizuri zaidi maishani. Hivyo ni kusema elimu huondoa umaskini nchini.

Kadhalika elimu husaidia katika vita vya kupigana na maradhi. Watu walioelimika huelewa kanuni za afya vizuri. Hula lishe bora na wanao uwezo wa kugharamia matibabu. Aidha, elimu hufanya nchi iwe na madaktari wa kutosha na vilevile huwezesha utafiti kuhusu magonjwa ufanyike na dawa kugunduliwa.

Ongezeko la haraka la idadi ya watu pamoja na vifo vya mapema hupunguzwa na elimu. Kwa kiasi fulani, uhalifu pia hupunguzwa na elimu. Kisiasa, elimu huimarisha umoja wa kitaifa, pia huwawezesha raia kujua haki zao. Mambo haya huchangia haki zao. Mambo haya huchangia demokrasia nchini. Kwa watu binafsi elimu huwapa ujuzi, ustadi na huwakuza kiakili. Elimu hujenga watu **<u>kihulka</u>** kama vile kimavazi, mahusiano yao na watu wengine na mawasiliano yao kwa ujumla.

Waledi wa Konga mawe hawakuenda mvange walipotanabahi kuwa elimu haina mwisho. Hivyo ni muhimu kila mmoja kujibidisha kila uchao kujielimisha zaidi. Jambo hilo lingemfanya yeyote anayehusika kuwa na uwezo mkubwa wa kukabiliana na maisha na pengine kuwa na mapato makubwa.

Kwa upande mwingine serikali hunufaika kutokana na kodi kubwa ya watu walio na mapato makubwa. Hii huchangia hazina ya taifa.

31. Ni jambo gani lisilo la kweli kuhusu elimu kati ya haya?
A. Elimu huondoa ufukara
B. Si shida kugharamia elimu
C. Elimu huwawezesha watu kupata ujira
D. Elimu ni mwanga wa taifa

32. Elimu huimarisha uchumi wa taifa kwa vile
A. watu walioelimika huzalisha rasilimali
B. watu hupata ujuzi na ustadi
C. nchi huwekeza katika elimu
D. hugharamiwa na serikali

33. Kuelewa kanuni za afya vizuri husaidia ______
A. kuponya maradhi
B. kupata maradhi
C. kusambaza maradhi
D. kuzuia maradhi

34. Utafiti huwezesha ______
A. kugundua dawa
B. kupata maradhi
C. kupata madaktari
D. kula lishe bora

35. Elimu huinua nchi ______
A. kuuchumi
B. kisiasa
C. kiuchumi
D. kijamii

36. Ni nini maana ya kuwekeza?
A. Kuwekelea
B. Kulipia elimu
C. Kuhimiza demokrasia
D. Kuzalisha mali

37. Ajira ni sawa na ______
A. uchumi
B. faida
C. kazi
D. pesa

38. Kisawe cha hulka ni ______
A. tabia
B. akili
C. sura
D. maendeleo

39. "Elimu ni bahari" ni mfano wa ______
A. tashbihi
B. istiari
C. msamiati
D. methali

40. Kichwa kinachofaa zaidi kwa habari hii ni ______
A. Elimu na serikali
B. Elimu na habari
C. Elimu na maisha
D. Elimu na maendeleo

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali ya 41 - 50.</u>***

Ama kwa kweli moyo wangu ulidunda kama ngoma. Nilijaribu kadri ya uwezo wangu kutowaza angalau nipate hata lepe la usingizi lakini **<u>niliambulia patupu</u>**. Nilitamani kusikia ndege wakiimba nyimbo zao za kuongoa-ongoa lakini wapi? Usingizi ulinipaa kabisa nikabaki nimetumbua macho tu ungedhani ni mjusi aliyebanwa na mlango. Nilihisi kana kwamba kichwa changu kingepasuka wakati wowote.

Muda ulizidi kusonga, akilini mwangu nilikuwa nikiwaza jinsi nilivyoanza masomo yangu ya msingi kutoka chekechea hadi darasa la nane katika shule ya msingi ya Kapecha. Katika darasa la nane mwalimu wetu mpendwa B.W Jambo alitukumbusha kubukua na kutalii matopa ya vitabu vya madarasa ya nyuma. Ilitubidi tutii na kufuata maagizo yake kwa sababu wakati wa kujua mbivu na mbichi ulikuwa umewadia.

Muda si ayami, jua lilichomoza, nami nikajizoazoa katika samadarini kuelekea sebuleni. Nilikuwa na kiwewe kwani kwa mintaarafu ya waziri wa elimu, matokeo yangetangazwa punde. Niliketi kwenye kiti huku nimeishiwa na nguvu kama mja aliyechoka tiki. Wazazi wangu walipojihimu walinipata kitini nikiwa nimenyong'onyea hayati si mamati, walifahamu kilichokuwa kimenisibu na kwa hivyo hawakuchelewa kunirai kwamba nisiwe na jakamoyo kwani nilikuwa nimepita.

Adhuhuri ilipowadia, taarifa kuu zilikuwa ni "Matokeo ya Mtihani wa K.C.P.E 2020/2021." Nilitega masikio ndi na kuyafungua macho yangu yote kutazama kila tukio. Baada ya waziri Profesa Magoha kutoa hotuba fupi kuhusu yaliyotokea wakati wa kufanywa kwa mitihani hiyo, alianza kwa kutaja mwanafunzi aliyekuwa wa kwanza nchini; amini usiamini, sadiki ukipenda. Jina langu lilitajwa la kwanza.

Wazazi wangu hawakuamini sembuse mimi? Billahi! Nilijua kuwa ningefanya vyema lakini sikuliwazia kuwa ningekuwa mwanafunzi wa kwanza nchini. Yaumu hiyo hiyo wanahabari na mheshimiwa mbunge wetu waliwasili nyumbani kwetu kwa mlolongo wa magari. Waliyaegesha magari yao na kutoka nje kumwona shujaa huyu aliyeibuka nambari moja kutoka shule ndogo iliyo katika kiambo kidogo cha Jomvu. Wote walikuwa wamevaa tabasamu swadakta nyusoni mwao ungedhani yalikuwa maua ya waridi katika unyevu wa asubuhi. Furaha iliyoje?

Wageni hawa wote walishangaa walipoitazama nyumba yetu ya msonge iliyokuwa imejiinamia kama mbavu za mbwa. Walitaka sana niwaeleze jinsi nilivyojimudu hadi nikafikia mahali nilipokuwa kuwapita wanagenzi wengine nchini. Bila maficho, niliwafungulia moyo wangu na kuwaelezea kila kitu. Awali kabisa niliwaambia kwamba ni sharti mtu amweke Dayani mbele na kujifunga kibwebwe katika kila jambo. Inna, bidii hulipa aidha Mcha Mungu si mtovu.

41. Maneno ambulia patupu ni sawa na
   A. kutoka kupata usingizi
   B. kukosa ulichofarajia
   C. kulala kupita kiasi
   D. kuwa na mawazo mengi

42. Ni kwa nini mwandishi hakuweza kulala?
   A. Alikuwa akisoma kuukalia mtihani wake
   B. Alikuwa awapokee wageni kwao
   C. Aliwaza kuhusu matokeo ambayo yangetangazwa keshoye
   D. Hakuona haja ya kulala kabisa

43. Msingi wa matokeo yake mazuri, mwandishi anasema ulitokana na nini?
   A. Kumwamini Mungu, kufanya bidii na kujiamini
   B. Kufanya bidii na kuamka mapema
   C. Kulala kuchelewa na kusoma kwa bidii
   D. Kujifunga kibwebwe, kuwatii walimu na kudurusu kazi ya darasa la nane

44. Ni wakati gani ambapo mwandishi alipata usingizi?
   A. Jua lilipochomoza
   B. Ndege walipoimba
   C. Wazazi walipoamka
   D. Hakupata usingizi

45. Kulingana na aya ya tatu, ni sahihi kusema kuwa ________
   A. mwandishi alikuwa mwenye mawazo mengi
   B. mwandishi aliugua kutokana na kukosa usingizi
   C. mwandishi alionekana mnyonge kana kwamba alikuwa mgonjwa
   D. wazazi wake mwandishi waliamka mapema kabla ya yeye kuamka

46. Kabla ya kutangaza matokeo rasmi waziri wa elimu, ________
   A. alitangaza orodha ya waliofanya vizuri
   B. alitoa hotuba kuhusu yaliyofanyika wakati wa mtihani
   C. alizungumzia zaidi kuhusu shule zilizofanya vyema
   D. alimkaribisha mwandishi kuzungumza na wanahabari

47. Neno sembuse limetumika katika taarifa hii, hutumika
   A. kulinganisha vitu au matukio mawili ili kuonyesha tofauti iliyopo
   B. kuunganisha sentensi mbili ndefu
   C. unapotaka kupishwa njia upite
   D. unapotaka kujua jibu la swali fulani

48. Ni kwa nini mwandishi alishtuka sana alipotajwa kuwa mwanafunzi wa kwanza nchini?
   A. Jina lake kutajwa na waziri wa elimu
   B. Kutambua kuwa alikuwa wa kwanza nchini
   C. Kuwaona wanahabari wengi kufika kwao
   D. Wanahabari kujua kuwa alitoka familia maskini

49. Ni dhahiri kusema kuwa familia ya mwandishi
   A. ilikuwa tajiri sana
   B. ilikuwa imeheshimika na wote
   C. ilijulikana na watu wote nchini
   D. ilikuwa ya kiwango cha chini cha maisha

50. Ni methali gani inayojitokeza kulingana na makala haya?
   A. Bidii hulipa
   B. Mwenye nguvu mpishe
   C. Maskini hana haki
   D. Mwenda tezi na omo marejeo ni ngamani